

Wazazi wangu hawajaunganishwa hekaluni. Je, hiyo inamaanisha siwezi kuwa sehemu ya familia ya milele?  
–Mtu anayejiuliza akiwa Warsaw

## Mpendwa Unayejiuliza,

Wewe ni mtoto wa wazazi wa mbinguni. Hata kabla hujaja kwenye dunia hii, ulikuwa sehemu ya familia Yao. Na hilo halitabadilika kamwe! Hivyo, lolote liwalo, daima utakuwa sehemu ya familia ya milele! Baba wa Mbinguni anawapenda sana wewe na familia yako. Anawataka nyote mrejee Kwake. Ataendelea kuwabariki na kuwaongoza wewe na familia yako. Sali Kwake kuhusu wasiwasi wako na Yeye atakufariji. Kwa upendo,  
Gazeti la *Rafiki*

Mchore kila mmoja wa wanafamilia yako na jambo unalolipenda kuwahusu! Tafuta mema katika familia yako. Waambie kile unachokiona!

### Mimi na Familia Yangu

Familia yako ni zaidi ya wewe na wazazi wako. Familia yako ni bibi na babu zako, binamu zako na wale wote waliokutangulia. Siku moja familia yako inaweza kujumuisha mwenza wako na watoto wako. Hiyo ni familia moja kubwa!